# NA. 04: TOLEO LA TAKWIMU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII - ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRIL HADI JUNI, 2025

## 1.0 Utangulizi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia katika kuimarisha takwimu za Matukio ya Kijamii. Miongoni mwa takwimu hizo ni takwimu za Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka.

Toleo la robo ya pili ya mwaka 2025 (Aprili-Juni), linatoa muhtasari wa takwimu za Matukio ya kijamii. Takwimu hizi zinatolewa kwa kulinganisha kijiografia (Wilaya) na kijinsia. Takwimu za Matukio ya Kijamii hutoa taarifa za idadi ya matukio ya kijamii yaliyosajiliwa na Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## 2.0 Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za Usajili wa Matukio ya Kijamii za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya kijamii, kupima mafanikio ya Sera za Afya na kutambua changamoto za kijamii. Aidha, takwimu za matukio ya Kijamii husaidia katika kutathimini maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi, pia hutoa mwongozo muhimu kwa watafiti, serikali, na mashirika ya maendeleo katika kufanya tathimini na maamuzi sahihi kwa jamii. Toleo hili linawasilisha takwimu zifuatazo.

### 2.1 Usajili wa Vizazi hai

Jumla ya Vizazi hai 10,062 vimeripotiwa kusajiliwa kwa kipindi cha April hadi Juni, 2025, ambapo 5,183 (51.5%) ni wanaume na wanawake 4,879 (48.5%), usajili unaonesha kuwa uwiano wa jinsi ni wanawake 97 kwa kila wanaume 103. Aidha usajili umekuwa ukipungua kwa kila mwezi, ambapo mwezi wa Aprili 2025 vizazi 3,938 (39.14%) na kupungua hadi vizazi 3,612 (35.89%) kwa mwezi wa Mei 2025 na kupungua tena kwa mwezi wa Juni 2025, hadi kufikia 2,512 (24.97%) (Jadweli Na. 1).

Kwa kipindi cha Aprili-Juni 2025 usajili unaonesha kuwa, Wilaya ya Mjini imeripotiwa kusajili vizazi hai vingi zaidi ambavyo ni 2,557 (25.4%) ikifuatia na Wilaya ya Wete na Wilaya ya Magharibi ”B”ambazo zimeripoti kusajili vizazi

1,319 (13.1%) na 1,242 (12.34%) mtawalia. Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kusajili vizazi hai kidogo zaidi ambavyo ni 96 (0.95%) ukilinganisha na Wilaya nyingine.

**Jadweli Na. 1: Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Aprili-Juni 2025**

| Wilaya | April-2025 | | | May-2025 | | | Juni-2025 | | | April-Juni, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 129 | 152 | 281 | 141 | 125 | 266 | 107 | 124 | 231 | 377 | 401 | 778 |
| Kaskazini B | 28 | 23 | 51 | 10 | 17 | 27 | 8 | 10 | 18 | 46 | 50 | 96 |
| Kati | 71 | 70 | 141 | 66 | 53 | 119 | 43 | 50 | 93 | 180 | 173 | 353 |
| Kusini | 77 | 76 | 153 | 79 | 81 | 160 | 31 | 34 | 65 | 187 | 191 | 378 |
| Mjini | 492 | 416 | 908 | 486 | 450 | 936 | 363 | 350 | 713 | 1,341 | 1,216 | 2,557 |
| Magharibi A | 254 | 241 | 495 | 174 | 153 | 327 | 124 | 112 | 236 | 552 | 506 | 1,058 |
| Magharibi B | 298 | 268 | 566 | 266 | 256 | 522 | 83 | 71 | 154 | 647 | 595 | 1,242 |
| Micheweni | 170 | 178 | 348 | 215 | 214 | 429 | 130 | 101 | 231 | 515 | 493 | 1,008 |
| Wete | 271 | 244 | 515 | 219 | 202 | 421 | 203 | 180 | 383 | 693 | 626 | 1,319 |
| Chakechake | 153 | 138 | 291 | 126 | 113 | 239 | 136 | 118 | 254 | 415 | 369 | 784 |
| Mkoan | 82 | 107 | 189 | 83 | 83 | 166 | 65 | 69 | 134 | 230 | 259 | 489 |
| **Jumla** | **2,025** | **1,913** | **3,938** | **1,865** | **1,747** | **3,612** | **1,293** | **1,219** | **2,512** | **5,183** | **4,879** | **10,062** |

### 2.1.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi Hai, Januari - Mach 2025 na April-Juni 2025

Katika kipindi cha Januari – Machi 2025, usajili wa vizazi hai ulikuwa mkubwa kwa jumla ya vizazi 11,618, huku wanaume wakiwa 5739 (49.4%) na wanawake 5879 (50.6%). Wilaya ya Mjini ndiyo iliyosajili vizazi vingi zaidi ambavyo ni 2,623 (22.6%), ikifuatiwa na Micheweni 1,491 (12.8%) na Wete 1,282 (11.0%) huku Wilaya ya Kusini, Kati na Kaskazini B zikisajili idadi ndogo (chini ya vizazi 500 kwa kila Wilaya).

Kwa upande wa Aprili – Juni 2025, kulikuwa na kupungua kwa usajili wa vizazi hai, ambapo jumla ya vizazi 10,062 vilisajiliwa, hii ni sawa na upungufu wa usajili wa vizazi 1,556 (15.46%) ikilinganishwa na robo mwaka ya mwanzo wa mwaka 2025 (Januari – Machi 2025). Upungufu zaidi unaonekana katika Wilaya ya Kasikazini "B" ikiwa imesajili jumla ya vizazi 96 (0.95%), Wilaya ya Kati ikisajili jumla ya vizazi 353 (3.5%) na Wilaya ya Kusini imesajili jumla ya vizazi 378 (3.8%). Kupungua huku kwa usajili wa vizazi kunatoa ishara ya watu kutokuhamasika kufanya usajili wa matukio ya kijamii.

**Jadweli Na. 2: Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Jan- Machi 2025 na Apri-Juni 2025**

| Wilaya | Januari-Machi, 2025 | | | April-Juni, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 484 | 603 | 1,087 | 377 | 401 | 778 |
| Kaskazini B | 115 | 128 | 243 | 46 | 50 | 96 |
| Kati | 223 | 268 | 491 | 180 | 173 | 353 |
| Kusini | 223 | 227 | 450 | 187 | 191 | 378 |
| Mjini | 1,368 | 1,255 | 2,623 | 1,341 | 1,216 | 2,557 |
| Magharibi A | 474 | 461 | 935 | 552 | 506 | 1,058 |
| Magharibi B | 491 | 484 | 975 | 647 | 595 | 1,242 |
| Micheweni | 767 | 724 | 1,491 | 515 | 493 | 1,008 |
| Wete | 632 | 650 | 1,282 | 693 | 626 | 1,319 |
| Chakechake | 421 | 535 | 956 | 415 | 369 | 784 |
| Mkoani | 541 | 544 | 1,085 | 230 | 259 | 489 |
| **Jumla** | **5,739** | **5,879** | **11,618** | **5,183** | **4,879** | **10,062** |

Kwa ujumla, tofauti kubwa kati ya vipindi hivi viwili inaashiria kutokuimarika kwa upatikanaji wa huduma za usajili wa vizazi hai. Aidha, upungufu huu unaweza kuwa ni matokeo ya kutohamasika kwa jamii kwa kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka 2025 juu ya umuhimu wa usajili wa vizazi kwa ajili ya huduma za jamii (elimu na afya) na kisheria (Vitambulisho ZanID na NIDA).

### 2.1.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi Hai, Aprili – Juni, 2024 na Aprili-Juni, 2025

Katika kipindi cha Aprili - Juni 2024, usajili wa vizazi hai ulikuwa wa kiwango cha chini kwa jumla ya vizazi 9,150 huku wanaume wakiwa 4,219 (46.1%) na wanawake 4,931 (53.9%). Kwa upande wa Aprili - Juni 2025, usajili wa vizazi hai, ulikuwa juu ukilinganishwa na robo mwaka kama hiyo katika mwaka 2024 ambapo jumla ya vizazi 10,062 vilisajiliwa, ikijumuisha wanawaume 5,183 (51.5%) na wanawake 4,879 (48.5%). Kwa kipindi cha April – Juni kuna ongezeko la vizazi 912 (10%).

Ongezeko hilo linaonekana zaidi katika Wilaya ya Mjini (kutoka vizazi 1352 kwa April - Juni, 2024 hadi vizazi 2557 kwa April – Juni, 2025), Magharibi A (kutoka vizazi 281 kwa April - Juni, 2024 hadi vizazi 1058 kwa April – Juni, 2025), Magharibi B (kutoka vizazi 739 kwa April - Juni, 2024 hadi vizazi 1242 kwa April – Juni, 2025), Micheweni (kutoka vizazi 613 kwa April - Juni, 2024 hadi vizazi 1008 kwa April – Juni, 2025), na Wete (kutoka vizazi 762 kwa April - Juni, 2024 hadi vizazi 1319 kwa April – Juni, 2025).

Kuongezeka huku kwa usajili ya vizazi kunaashiria maendeleo ya mfumo wa usajili, ukubwa wa usajili na ukaribu pamoja na urahisi wa upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Hii inaleta faida kwa watoto kupata utambulisho kamili na kuiwezesha serikali kupanga maendeleo, kutoa huduma na kusimamia rasilimali zao kwa urahisi.

**Jadweli Na. 3: Mlinganisho wa Usajili wa Vizazi hai kwa Jinsi na Wilaya, Aprili- Juni, 2024 na Apri-Juni, 2025**

| | April-Juni, 2024 | | | April-Juni, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 587 | 773 | 1,360 | 377 | 401 | 778 |
| Kaskazini B | 183 | 200 | 383 | 28 | 44 | 72 |
| Kati | 493 | 579 | 1,072 | 180 | 174 | 353 |
| Kusini | 253 | 207 | 460 | 187 | 191 | 378 |
| Mjini | 535 | 817 | 1,352 | 1,341 | 1,216 | 2,557 |
| Magharibi A | 137 | 144 | 281 | 552 | 506 | 1,058 |
| Magharibi B | 355 | 384 | 739 | 647 | 595 | 1,242 |
| Micheweni | 279 | 334 | 613 | 515 | 493 | 1,008 |
| Wete | 351 | 411 | 762 | 693 | 626 | 1,319 |
| Chakechake | 441 | 385 | 826 | 415 | 369 | 784 |
| Mkoani | 605 | 697 | 1,302 | 230 | 259 | 489 |
| **Jumla** | **4,219** | **4,931** | **9,150** | **5,183** | **4,879** | **10,062** |

## 2.2 Usajili wa Vifo

Jumla ya Vifo 467 vimesajiliwa kwa kipindi cha miezi mitatu (Aprili – Juni, 2025), ambapo wanaume walikuwa ni 285 ( 61.0%) na wanawake ni 182 (39.0%). Aidha, uwiano wa vifo vilivyosajiliwa kwa jinsi ni wanaume 285 kwa wanawake 182, hii inaonesha kuwa usajili wa vifo kwa wanaume ni mkubwa ukilinganisha na wanawake (Jadweli Na.4). Usajili wa vifo umekuwa ukipungua kila mwezi ambapo kwa mwezi wa Aprili 2025 jumla ya vifo 181 (38.8%) vimesajiliwa na kupungua hadi kufikia vifo 156 (33.4%) mwezi Mei 2025 na kupungua zaidi hadi kufikia vifo 130 (27.8%) mwezi wa Juni 2025.

Katika kipindi cha Aprili -Juni 2025, Wilaya ya Mjini imesajili vifo vingi zaidi ambavyo ni jumla ya vifo 126 (26.98%), ikifuatiwa na Wilaya ya Mkoani iliyosajili vifo 51 (10.9%). Aidha, Wilaya ya Kaskazini "B" usajili wa vifo ni mdogo (12 sawa na asilimia 2.6) kwa kipindi cha Aprili – Juni 2025 ukilinganishwa na wilaya nyingine (Jadweli 4).

**Jadweli Na. 4: Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Aprili-Juni 2025**

| Wilaya | April-2025 | | | May-2025 | | | Juni-2025 | | | April-Juni, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 5 | 2 | 7 | 6 | 8 | 14 | 8 | 6 | 14 | 19 | 16 | 35 |
| Kaskazini B | 4 | 1 | 5 | 4 | 1 | 5 | 2 | 0 | 2 | 10 | 2 | 12 |
| Kati | 5 | 12 | 17 | 4 | 8 | 12 | 10 | 2 | 12 | 19 | 22 | 41 |
| Kusini | 6 | 4 | 10 | 6 | 3 | 9 | 6 | 2 | 8 | 18 | 9 | 27 |
| Mjini | 31 | 11 | 42 | 24 | 16 | 40 | 30 | 14 | 44 | 85 | 41 | 126 |
| Magharibi A | 16 | 7 | 23 | 7 | 4 | 11 | 5 | 6 | 11 | 28 | 17 | 45 |
| Magharibi B | 5 | 10 | 15 | 6 | 8 | 14 | 1 | 4 | 5 | 12 | 22 | 34 |
| Micheweni | 9 | 0 | 9 | 7 | 3 | 10 | 2 | 3 | 5 | 18 | 6 | 24 |
| Wete | 9 | 1 | 10 | 7 | 1 | 8 | 5 | 3 | 8 | 21 | 5 | 26 |
| Chakechake | 13 | 6 | 19 | 6 | 11 | 17 | 6 | 4 | 10 | 25 | 21 | 46 |
| Mkoani | 14 | 10 | 24 | 11 | 5 | 16 | 5 | 6 | 11 | 30 | 21 | 51 |
| Jumla | 117 | 64 | 181 | 88 | 68 | 156 | 80 | 50 | 130 | 285 | 182 | 467 |

### 2.2.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, April-Juni, 2024 na Januari-Machi 2025

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2025, jumla ya vifo 467 vilivyosajiliwa, ambapo wanaume walikuwa 285 (61.0%) na wanawake 182 (39.0%). Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa ambavyo ni 126 (27.0%), ikifuatiwa na Mkoani 51 (10.9%) na Chakechake 46 (9.9%). Wilaya ya Kaskazini B, na Micheweni ziliripoti idadi ndogo ya vifo vilivyosajiliwa ambavyo ni 12 (2.7%) na 24 (5.1%) mtawalia.

Aidha, usajili wa vifo unaonekana kuwa mkubwa zaidi kwa kipindi cha Januari - Machi 2025 kwa kufikia vifo 668 ukilinganisha na vifo 467 vilivyosajiliwa kwa kipindi cha April - Juni 2025, sawa na upungufu wa asilimia 30.1. Wilaya zinazoonesha upungufu zaidi wa usajili wa vifo, ni Mjini kutoka vifo 211 hadi vifo 126, Wilaya ya Magharibi B kutoka vifo 125 hadi vifo 34, na Wilaya ya Wete kutoka vifo 51 hadi vifo 26.

Aidha, kuliripotiwa ongezeko la usajili wa vifo kwa Wilaya ya Magharibi A (kutoka 44 hadi vifo 45) na Wilaya ya Kati (kutoka 30 hadi vifo 41) kwa kipindi cha (Januari - Machi 2025) hadi (April-Juni, 2025). Hali hii inawekana kuwa inatokana na kuwa na uwelewa mdogo wa jamii juu ya usajili wa vifo vinavyotokea katika jamii, juhudi zaidi za uhamasishaji kwa jamii zinahitajika.

**Jadweli Na. 5: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi Januari - Machi, 2025 na Aprili-Juni 2025**

| Wilaya | Januari - Mchi 2025 | | | April - Juni, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 26 | 12 | 38 | 19 | 16 | 35 |
| Kaskazini B | 8 | 7 | 15 | 10 | 2 | 12 |
| Kati | 20 | 10 | 30 | 19 | 22 | 41 |
| Kusini | 15 | 16 | 31 | 18 | 9 | 27 |
| Mjini | 109 | 102 | 211 | 85 | 41 | 126 |
| Magharibi A | 25 | 19 | 44 | 28 | 17 | 45 |
| Magharibi B | 68 | 57 | 125 | 12 | 22 | 34 |
| Micheweni | 25 | 9 | 34 | 18 | 6 | 24 |
| Wete | 30 | 21 | 51 | 21 | 5 | 26 |
| Chakechake | 30 | 18 | 48 | 25 | 21 | 46 |
| Mkoani | 28 | 13 | 41 | 30 | 21 | 51 |
| **Jumla** | **384** | **284** | **668** | **285** | **182** | **467** |

### 2.2.2 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Aprili-Juni, 2024 na Aprili-Juni, 2025

Katika kipindi cha Aprili - Juni 2024, usajili wa vifo ulikuwa wa kiwango cha juu kwa jumla ya vifo 1,230, huku wanaume wakiwa 684 (55.6%) na wanawake 546 (44.4%). Kwa upande wa Aprili - Juni 2025, usajili wa vifo, ulishuka ukilinganishwa na robo mwaka kama hiyo katika mwaka 2024 ambapo jumla ya vifo 467 vilisajiliwa, ikiwa ni sawa na upungufu wa vifo 763 (62.0%).

Upungufu huo zaidi umeonekana katika Wilaya ya Mjini ambapo usajili umeshuka kutoka vifo 765 kwa April-Juni, 2024 hadi vifo 126 kwa April-Juni, 2025. Hali hii inaashiria kuimarika kwa huduma za afya na kupunguza idadi ya vifo au uelewa mdogo wa jamii juu ya usajili wa matukio ya kijamii hususan usajili wa vifo.

**Jadweli Na. 6: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Aprili -Juni, 2024 na Aprili-Juni 2025**

| Wilaya | April – Juni 2024 | | | April - Juni, 2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 40 | 43 | 83 | 19 | 16 | 35 |
| Kaskazini B | 21 | 15 | 36 | 10 | 2 | 12 |
| Kati | 18 | 10 | 28 | 19 | 22 | 41 |
| Kusini | 5 | 8 | 13 | 18 | 9 | 27 |
| Mjini | 402 | 363 | 765 | 85 | 41 | 126 |
| Magharibi A | 25 | 30 | 55 | 28 | 17 | 45 |
| Magharibi B | 45 | 33 | 78 | 12 | 22 | 34 |
| Micheweni | 14 | 7 | 21 | 18 | 6 | 24 |
| Wete | 50 | 20 | 70 | 21 | 5 | 26 |
| Chakechake | 9 | 8 | 17 | 25 | 21 | 46 |
| Mkoani | 55 | 9 | 64 | 30 | 21 | 51 |
| Jumla | 684 | 546 | 1,230 | 285 | 182 | 467 |

## 2.3 Usajili wa Ndoa

Jumla ya Ndoa 3,871 zimesajiliwa kwa kipindi cha Aprili - Juni, 2025, jumla ya ndoa 1,111 (28.7%) zimefungwa na kusajiliwa mwezi wa Aprili 2025, na kuongezeka hadi kufikia ndoa 1,364 (35.2%) mwezi Mei, 2025 na kuongezeka tena hadi kufikia ndoa 1,396 (36.0%) zilizosajiliwa kwa mwezi wa Juni 2025 (Jadweli Na. 7).

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa Wilaya ya Magharibi "B" imesajili ndoa nyingi zaidi ambazo ni 1,135 (29.3%), ikifuatia na Wilaya ya Mjini na Magharibi A ambazo zimeripoti kusajili ndoa 904 (23.3%) na 822 (21.2%) mtawalia. Aidha, kwa kipindi cha Aprili – Juni 2025 Wilaya ya Mkoani imeripotiwa kusajili ndoa kigogo zaidi ambayo ni moja tu (0.03%) ikifuatiwa na Wilaya ya Wete ndoa 33 (0.9%) na Wilaya ya Micheweni ndoa 40 (1.0%). Hii inaashiria mwamko mdogo wa jamii juu ya usajili wa ndoa ukilinganisha na ndoa zinazofungwa katika jamii.

**Jadweli Na. 7: Usajili wa Ndoa kwa Wilaya, Aprili – Juni 2025**

| Wilaya | April-2025 | May-2025 | Juni-2025 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 77 | 111 | 74 | 262 |
| Kaskazini B | 15 | 87 | 48 | 150 |
| Kati | 51 | 48 | 48 | 147 |
| Kusini | 63 | 55 | 67 | 185 |
| Mjini | 267 | 328 | 309 | 904 |
| Magharibi A | 231 | 255 | 334 | 820 |
| Magharibi B | 318 | 351 | 466 | 1,135 |
| Micheweni | 6 | 18 | 16 | 40 |
| Wete | 8 | 13 | 12 | 33 |
| Chakechake | 75 | 97 | 22 | 194 |
| Mkoani | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Jumla | 1,111 | 1,364 | 1,396 | 3,871 |

## 2.4 Usajili wa Talaka

Jumla ya Talaka 374 zimesajiliwa kwa kipindi cha Aprili–Juni, 2025. Jumla ya talaka 122 (32.6%) zimesajiliwa kwa mwezi Aprili 2025 na Mei 2025 kwa kila mwezi, na mwezi Juni 2025 usajili wa talaka umeongezeka hadi kufikia talaka 130 (34.8%) kama zinavyoonekana kwenye Jadweli Na. 8.

Aidha, Wilaya ya Magharibi "B"imeripoti kusajili idadi kubwa zaidi ya talaka ambazo ni 119 (31.8%) ikilinganishwa na Wilaya nyingine kwa kipindi cha April-Juni 2025, ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini iliyoripotiwa kusajili Talaka 68 (18.2%) na wilaya ya Kati ilisajili talaka 58 (15.5%). Bado kuna mwamko mdogo wa usajili wa talaka kwa jamii, hali hii inaonekana kuwa kubwa zaidi katika Wilaya ya Mkoani, Micheweni na Wete ambazo hazikuwa na usajili kabisa wa talaka katika kipindi cha Aprili-Juni 2025.

**Jadweli Na. 8: Usajili wa Talaka kwa Mwezi, Aprili - Juni 2025**

| Wilaya | April-2025 | May-2025 | Juni-2025 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 15 | 7 | 7 | 29 |
| Kaskazini B | 2 | 4 | 0 | 6 |
| Kati | 22 | 15 | 21 | 58 |
| Kusini | 8 | 3 | 11 | 22 |
| Mjini | 11 | 34 | 23 | 68 |
| Magharibi A | 1 | 5 | 14 | 20 |
| Magharibi B | 38 | 27 | 54 | 119 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 25 | 27 | 0 | 52 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 122 | 122 | 130 | 374 |

## 3.0 Hitimisho

Kwa ujumla, taarifa za matukio ya kijamii ni muhimu sana kwa kuimarisha huduma za kijamii, kuleta mabadiliko chanya, na kukuza ustawi wa jamii. Jamii inapaswa kushiriki kikamilifu katika kusajili matukio ya kijamii kwa maendeleo ya Taifa.

Ikumbukwe kuwa takwimu zilizowasilishwa hapa ni zile tu zilizosajiliwa rasmi kupitia Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA). Kuna matukio mengi kwenye jamii hasa ya vifo na talaka ambayo yanatokea katika jamii na hayasajiliwi rasmi. Aidha, jamii inasisitizwa kuwa na utamaduni wa kusajili matukio ya Kijamii kwa mamlaka husika ili yaweze kusajiliwa, na kuisaidia serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kupanga mipango yenye tija kwa taifa.

## Maelezo Muhimu

- Kizazi hai ni tukio la mtoto kuzaliwa akiwa hai, yaani, mtoto ambaye amezaliwa ana pumzi, anafanya harakati, na ana ishara za maisha. Kizazi hai mara nyingi hufuatana na mchakato wa kawaida wa kujifungua, ambapo mtoto huzaliwa kuja ulimwenguni.

- Kifo ni tukio la mwisho la kuishi. Ni tukio ambalo mwili huacha kabisa kufanya kazi kwa binadamu, kifo hutokea wakati moyo unasimama na kusitisha mtiririko wa damu mwilini, na ubongo kusimama kufanya kazi.

- Sheria Namba 3 ya 2018, inaeleza kuwa Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ina majukumu ya kusajili Matukio ya kijamii na kutoa vyeti maalum, matukio hayo ni Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na Wasiokua Wazanzibari

Wakaazi.

- Sheria Namba 9 ya mwaka 2007 inaeleza kuwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia uendeshaji wa kazi za takwimu katika taasisi zote za Serikali na binafsi zinazofanya shughuli zake hapa Zanzibar.

***Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:***

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI,**
P.O.Box 2321, Zanzibar
7 Barabara ya Fumba
71125 Mjini Magharibi
Email: info@ocgs.go.tz
Phone: +255 242240134
Fax: +255 242240135
http://www.ocgs.go.tz

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMI**
Simu: +255 772 400 597
S.L.P: 264
Barua pepe: info@zcsra.go.tz
Flamingo, Migombani Zanzibar Tanzania.